“WARAKA NA.055/2017 (MASHARTI YA KUFANYA BIASHARA NA MAKAMPUNI YA BIMA MTAWANYO NA MADALALI WA BIMA MTAWANYO KUTOKA NJE YA NCHI)”

KWA: **MAKAMPUNI YOTE YA BIMA NCHINI**

YAHUSU: **MASHARTI YA KUFANYA BIASHARA NA MAKAMPUNI YA BIMA MTAWANYO NA MADALALI WA BIMA MTAWANYO KUTOKA NJE YA NCHI**

TAREHE: **11 DISEMBA, 2017**

TOLEO: **TOLEO LA MWISHO**

1. Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima nchini (TIRA) imeamua kuangalia upya vigezo vinavyohusu taratibu za bima mtawanyo kwa makampuni ya bima yaliyosajiliwa kufanya biashara za bima ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kulingana na kifungu Na. 31(2) cha Sheria ya Bima ya mwaka 2009 pamoja na sehemu ya VII (Bima Mtawanyo za lazima) ya sheria ya Bima.

2. Kifungu Na. 31(2) cha Sheria ya Bima ya mwaka 2009 kinaeleza kuwa ***“utekelezaji wa taratibu zote za bima mtawanyo na bima za kawaida utafanyika kwa mwongozo wa Kamishna wa Bima”.***

3. Mamlaka imebaini, matumizi yasiyo sahihi ya taratibu za bima mtawanyo kwa baadhi ya makampuni ya bima, kama ifuatavyo:

    (i) Matumizi yaliyopindukia ya taratibu za kimataifa za bima mtawanyo za makubaliano ya papo-kwa-papo *(“International Facultative Reinsurance Arrangements”)* hata kwenye mazingira ambayo biashara husika zingeweza kufanyika kwa njia ya bima mtawanyo ya mikataba *(“Treaty Reinsurance Arrangements”)*;

(ii) Upelekwaji wa biashara ya bima kwa asilimia mia moja nje ya nchi ("fronting of risks") ambapo sehemu yake ingeweza kubakizwa nchini;
(iii) Ushiriki hafifu wa makampuni ya bima nchini katika kutoa bima za majanga makubwa na magumu (large and complex risks);
(iv) Baadhi ya makampuni ya bima nchini kupendelea kushirikisha makampuni tanzu yaliyo nje ya nchi katika kutoa kinga za bima nchini badala ya kushirikisha makampuni ya bima ya hapa nchini *("co-insurance arrangements with sister or parent companies based in other jurisdictions");*
(v) Baadhi ya makampuni ya bima nchini kufanya biashara za bima na makampuni ya bima mtawanyo yasiyo na viwango bora vya ithbati;
(vi) Kufanya biashara na makampuni ya bima mtawanyo na madalali wa bima mtawanyo nje ya nchi bila kuzingatia hali zao kisheria, kiutendaji na kifedha;
(vii) Kukosekana kwa uwazi kuhusu viwango na mahali zinapolipwa ada na kamisheni za bima panapotumika mlolongo wa madalali wa bima mtawanyo;
(viii) Baadhi ya makampuni ya bima kuomba kupeleka nje ya nchi biashara za bima ambazo muda wake umekwisha au unakaribia kwisha; na
(ix) Kukosekana kwa uwazi wa kutosha kuhusu mapato (ada na kamisheni) yatokanayo na biashara ya bima kupelekwa nje ya nchi ("*reinsurance commission/ fronting fee*").

4. Dhumuni la waraka huu ni **kuimarisha usimamizi wa matakwa ya kifungu Na. 31(2) na sehemu ya VII ya sheria za bima** kwa kuhakikisha makampuni ya bima yanafanya biashara ipasavyo kwenye eneo la bima mtawanyo. **Hivyo, mambo yafuatayo yazingatiwe:**

5. **Mikataba na taratibu zote za bima mtawanyo kati ya makampuni ya bima nchini na makampuni ya bima mtawanyo yaliyoko nje ya nchi ni lazima zipate kibali cha Mamlaka kabla**

ya utekelezaji. Hivyo basi, rasimu za mikataba yote ya bima mtawanyo ("draft reinsurance treaties") ni lazima iwe imewasilishwa katika ofisi za Mamlaka kabla au ifikapo tarehe 30 Septemba kila mwaka kwa ajili ya ukaguzi na kuidhinishwa.

6. **Hakutakuwa na upelekwaji wa biashara za bima nje ya nchi kwa asilimia mia (fronting)**, isipokuwa kwa masharti yafuatayo:

   (i) Kampuni ya bima ibakize nchini kiasi **kinacholingana na 5% au zaidi ya thamani ya mtaji wake** ("***shareholders' fund"*) kwa kila biashara ya bima iliyokusudiwa kupelekwa nje ya nchi**;

   (ii) Pale ambapo upelekwaji wa biashara ya bima nje ya nchi kwa asilimia mia hauepukiki kutokana na ukubwa au ugumu wake (size or complexity); biashara husika ni lazima ipitishwe kwa kampuni ya bima mtawanyo iliyosajiliwa nchini.

7. **Ujumuishaji usiofaa wa aina mbalimbali za bima *("irregular bundling and repackaging of risks")* kwa lengo la kuleta utatanishi na hivyo kuhamasisha upelekwaji wa biashara za bima nje ya nchi pasipo ulazima utahesabika kuwa ni kosa kisheria.**

8. **Uundwaji wa mifuko ya pamoja ya kukabiliana na majanga makubwa ya bima ("insurance pools")**: Makampuni ya bima nchini yanatakiwa kuunda mifuko ya pamoja ya kukabiliana na athari za majanga makubwa Kwa kusudio la kuimarisha uwezo wa soko kuandikisha na kubakiza sehemu kubwa ya biashara ya bima nchini ("market retention").

9. **Makampuni ya bima yasiyokidhi viwango vya kisheria vya ukwasi hayataruhusiwa kupeleka biashara ya bima nje kwa njia ya bima mtawanyo ya papo kwa papo ("facultative reinsurance"), isipokuwa kwa sababu maalum itakayoruhusiwa na Kamishna wa Bima.** Ukosefu wa ukwasi unaiweka kampuni ya bima katika hatari ya kufutiwa usajili au kuwekewa ukomo

wa kibiashara. Hali hiyo inamuacha mlaji wa bima kwenye hatari ya kukosa fidia pale janga linapotokea.

10. **Matumizi ya uwiano unaoridhisha wa makampuni ya bima mtawanyo:** Makampuni ya bima lazima yahakikishe kuwa yanatumia uwiano unaoridhisha wa makampuni ya bima mtawanyo.

11. **Uhusishwaji wa makampuni ya bima mtawanyo yaliyotathminiwa**: Makampuni ya bima mtawanyo yanayotumiwa na makampuni ya bima nchini ni lazima yawe na uwezo wa kifedha na yawe yametathminiwa kwa daraja la B+ au zaidi (au inayolingana nayo) na makampuni ya uthamini yanayoaminika kimataifa (reputable credit rating agencies).

12. **Utumiaji wa madalali wa bima mtawanyo waliosajiliwa nchini**:

    (i) Kila kampuni ya bima inayohitaji kupeleka biashara ya bima nje ya nchi inapaswa kutumia huduma za madalali wa bima waliosajiliwa nchini kati ya mteja wa bima na kampuni ya bima[1];
    (ii) Kila kampuni ya bima inayohitaji kupeleka biashara ya bima nje ya nchi inapaswa kutumia huduma za madalali wa bima mtawanyo waliosajiliwa nchini kati ya kampuni ya bima na makampuni ya bima mtawanyo;
    (iii) Huduma za dalali wa bima mtawanyo aliyesajiliwa nje ya nchi zitaweza kutumika pale tu ambapo dalali wa bima mtawanyo aliyesajiliwa nchini hawezi au hayuko tayari kushiriki, hivyo italazimu **kipengele cha 13** hapa chini kizingatiwe.

13. **Masharti ya kutumia madalali wa bima mtawanyo waliosajiliwa nje ya nchi**: Madalali wote waliosajiliwa nje ya nchi wanaohitaji kufanya biashara ya bima na makampuni ya bima

[1] Dalali wa bima ya kawaida haruhusiwi kuufanya shughuli za dalali wa bima mtawanyo au vinginevyo.

yaliyosajiliwa nchini ni **lazima yapate hati ya ithbati toka TIRA** ambayo itatolewa kwa muombaji anayekidhi vigezo vifuatavyo:

a) Kujaza fomu maalum ya maombi na kuiwakilisha TIRA;
b) Kutoa uthibitisho wa vielelezo vifuatavyo:
   (i) Usajili kwenye nchi anakotoka;
   (ii) Ushahidi wa usimamizi wa mwombaji na mamlaka ya bima katika nchi anakotoka;
   (iii) Taarifa za mahesabu ya kiuhasibu yaliyokaguliwa kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita;
   (iv) Taarifa zozote ambazo zitafaa kuwasilishwa TIRA; na
c) Malipo ya ada ya mwaka kiasi cha Dola za Kimarekani 5,000/=.

14. **Vigezo vya kufanya biashara na makampuni ya bima mtawanyo yaliyosajiliwa ndani ya nchi**[2]: Makampuni yote ya bima mtawanyo yaliyosajiliwa nje ya nchi yanayohitaji kufanya biashara na makampuni ya bima yaliyosajiliwa nchini ni **lazima yapate hati ya ithbati kutoka TIRA** ambayo itatolewa kwa muombaji anayekidhi vigezo vifuatavyo:

a) Kujaza fomu maalum ya maombi na kuiwakilisha TIRA;
b) Kutoa uthibitisho wa vielelezo vifuatavyo:
   (i) Usajili kwenye nchi anakotoka;
   (ii) Ushahidi wa usimamizi wa mwombaji na mamlaka ya bima katika nchi anakotoka;
   (iii) Daraja la uthaminishwaji na wakala huru inayotoa tathmini;
   (iv) Ushahidi wa usimamizi wa mwombaji na mamlaka ya bima katika nchi anakotoka;
   (v) Taarifa zozote ambazo zitafaa kuwasilishwa TIRA; na
c) Malipo ya ada ya mwaka kiasi cha Dola za Kimarekani 10,000/=.

[2] Vigezo vya kipengele cha 14 havitatumika kwa makampuni ya bima mtawanyo zilizoanzishwa kwa mikataba, sheria ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama au inamiliki hisa moja kwa moja au kupitia taasisi zingine

15. Kampuni ya bima ni lazima ihakikishe ina **wafanyakazi wenye utaalamu** wa kusimamia taratibu za bima mtawanyo.

16. **Kutii matakwa ya kisheria kuhusu bima mtawanyo za lazima:** Kampuni ya bima ni lazima ihakikishe kwamba matakwa ya sehemu ya VII ya sheria ya bima yanazingatiwa.

17. **Kima cha chini cha tozo ya bima inayolipwa TIRA kwa bima mtawanyo zinazopelekwa nje ya nchi:**

(i) Kampuni ya bima itapaswa kulipa tozo kwa kila bima mtawanyo itakayoruhusiwa na TIRA kwenda nje ya nchi kwa kiasi cha asilimia tatu (3%) ya ada ghafi *("gross premium")* au Dola za Kimarekani 200, yoyote itakayokuwa kubwa zaidi ya nyingine;

(ii) ***PAMOJA NA*** asilimia ishirini (20%) ya kiasi cha pato (fronting fee/ reinsurance commission) linalozidi asilimia kumi na mbili (12%).

18. **Matumizi ya uwezo wa soko la nchini kabla ya kupeleka biashara ya bima nje ya nchi:**

(i) Kila kampuni ya bima inatakiwa kushirikisha makampuni mengine ya bima nchini katika kutoa sehemu ya kinga ya bima kabla ya kupeleka sehemu inayobaki nje ya nchi;

(ii) Nyaraka zinazopaswa kutumwa TIRA (kama uthibitisho wa kushirikisha makampuni mengine ya bima nchini) ni pamoja na fomu husika toka TIRA zilizojazwa ipasavyo kutoka kwa kila kampuni ya bima iliyosajiliwa nchini.

19. **Kufanya bima ya ushirikiano ("co-insurance") na kampuni ya bima iliyosajiliwa nje ya nchi hakutaruhusiwa.** Bima za ushirikiano ni lazima zifanywe kati ya makampuni ya bima yaliyosajiliwa humu nchini.

20. **Ushirikiano miongoni mwa makampuni ya bima wenye lengo la kufifisha ushiriki wa makampuni hayo katika kutoa bima nchini ni kosa kisheria litakaloadhibika chini ya Sheria ya**

Bima: Makampuni ya bima yanafahamishwa kuwa ushirikiano wowote utakaosababisha biashara ya bima kupelekwa nje nchi pasipo ulazima wowote, ni kosa kisheria linaloadhibika kwa mujibu wa sheria.

21. **Ulazima wa Makampuni ya bima mtawanyo kutoa taarifa kuhusu makampuni ya bima mtawanyo yanayopokea biashara kutoka makampuni ya bima ya Tanzania:** Kila Kampuni ya bima nchini inatakiwa kuainisha makampuni ya bima mtawanyo ya nje yanayopokea biashara ya bima toka makampuni ya bima ya Tanzania**.**

22. **Bima ambazo muda wake umeisha hazitapelekwa nje ya nchi:** Hakuna kampuni ya bima itakayoruhusiwa kupeleka nje ya nchi bima ambayo muda wake umekwisha au muda mrefu umepita tokea bima ianze.

23. **Ulazima wa kutoa taarifa ya pato kwenye tozo na ada ya bima ("reinsurance commission/ fronting fees") linalolipwa kwa makampuni ya bima yaliyosajiliwa nchini:** Kila kampuni ya bima inatakiwa kutoa taarifa kuhusu pato linalopata kwa tozo ya bima kwa kila biashara ya bima inayopelekwa nje ya nchi.

24. **Kutojibu maombi ya makampuni mengine ya bima pale wanapoomba ushiriki wa katika kutoa sehemu ya bima ni kosa:** Kila kampuni ya bima inayoombwa na kampuni nyingine ya bima kushiriki katika kuchukua sehemu ya biashara ya bima inatakiwa ithibitishe kushiriki au kutoshiriki ndani ya siku 5 za kazi. Kutotoa uthibitisho kwa wakati ni kosa kisheria.

25. **Makampuni yote ya bima nchini yanayakiwa yafanyiwe tathmini za uwezo wao kifedha kuendelea kutoa huduma za bima ("credit rated")**: Kampuni ya bima iliyosajiliwa nchini ni lazimma itathminishwe angalau mara moja kila baada ya miaka mitatu.

26. **Biashara za bima za muda mrefu ("long-term assurance") hazitaruhusiwa kupelekwa nje ya nchi:**

(i) Hakuna biashara ya bima ya muda mrefu itakayoruhusiwa kupelekwa nje ya nchi;
(ii) Makampuni ya bima yanayofanya bima ya muda mrefu yanapaswa kushirikisha makampuni ya bima mtawanyo yaliyosajiliwa hapa nchini au kufanya ushirikiano na makampuni mengine ya bima yaliyosajiliwa nchini (co-insurance) au kuanzisha mifuko ya bima za aina hiyo au au kufanya taratibu nyingine zinazofanana na hizo.

27. **Muda wa kuanza kutumika kwa Waraka: Matakwa ya Waraka huu yataanza kutekelezwa kuanzia tarehe <u>1 Januari, 2018</u>.**

Ahsante kwa ushirikiano.

Dkt. Baghayo A. Saqware
Kamishna wa Bima

Nakala: 1. Mwenyekiti, Jumuiya ya akampuni ya Bima (ATI) – Kwa Utekelezaji;
2. Rais, Jumuiya ya Madalali wa Bima (TIBA) – Kwa Taarifa.